Tahadharini na madhambi yenye kudharauliwa

Kutoka kwa Sahal bin Sa'di Allah amridhie amesema: Amesema Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake: "Tahadharini na madhambi yenye kudharauliwa, kwani mfano wa madhambi yenye kudharauliwa, ni kama watu walioshuka chini ya bonde, akaja huyu na kijiti, na yule na kijiti, na akaja huyu na kijiti, mpaka wakaivisha mkate wao, na bila shaka madhambi yadharauliwayo akihesabiwa mfanyaji wake yanamuangamiza".

[Sahihi] [Imepokelewa na Ahmad]

Ametahadharisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake na kupuuza katika kuyafanya madhambi madogo, na kuyakithirisha kwani yanaangamiza yanapokuwa mengi, na akapiga mfano juu ya hilo wa watu walioshuka chini ya bonde, basi akaja kila mmoja wao na kijiti kidogo, mpaka wakaivisha mkate wao kwa mkusanyiko wa vile walivyovikusanya katika vijiti, na hakika madhambi yadharauliwayo pindi anapohesabiwa mfanyaji wake na akawa hajatubia kutokana na madhambi hayo au Mwenyezi Mungu amsamehe, basi humuangamiza.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/66224